**RISALA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAADILI NA HAKI ZA BINAADAMU ZANZIBAR,**
**TAREHE 16 DISEMBA, 2022**

**Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Zanzibar,**

**Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora,**

**Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid - Spika wa Baraza la Wawakilishi,**

**Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdalla, Jaji Mkuu wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi,**

**Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Talib Haji, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar,**

**Waheshimiwa Mawaziri,**

**Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Wabunge Mliopo,**

**Waheshimiwa Majaji wa Mahkama Kuu,**

**Viongozi mbalimbali wa Serikali na wa vyama mliohudhuria,**
**Wageni Waalikwa,**

**Ndugu Wananchi,**

**Mabibi na Mabwana.**

Asalaamu Aleykum.

Awali ya yote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema, uzima na nafasi ya kukutana kwa mara nyengine tena katika maadhimisho ya kilele cha Siku ya Maadili na Haki za Binadamu siku ya leo.

Pili, nachukua fursa hii kukushukuru **Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekeiti wa Baraza la Mapinduzi**, kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho haya ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu. Kuwepo kwako hapa katika maadhimisho haya ni uthibitisho wa juhudi zako katika kukuza na kuimarisha utawala bora hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Haya ni maadhimisho ya Sita ya Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu kufanyika Zanzibar ambapo kwa mara ya kwanza yalifanyika tarehe 10 Disemba, 2016 katika Viwanja vya Victoria Garden, Unguja. Tokea wakati huo, siku hii imekuwa ikiadhimishwa kila mwaka. Katika kipindi hiki cha miaka sita tokea Maadhimisho haya kuanza kufanyika, tarehe 10 Disemba mwaka 2018 Maadhimisho haya yalifanyika katika Viwanja vya Gombani Chake Chake, Pemba.

Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu yana umuhimu mkubwa katika kuimarisha misingi ya Utawala Bora nchini. Siku hii, kwa upande wetu, imejumuisha maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Kupambana na Rushwa Duniani na Siku ya Haki za Binaadamu Duniani. Siku hizo huadhimishwa Kimataifa

tarehe 9 na 10, *mtawalia,* ifikapo Disemba ya kila mwaka. Hata hivyo, kwa kuwa tarehe 9 Disemba Tanzania huwa ni siku ya Sherehe za Uhuru wa Tanganyika, Tanzania imeamua kuziadhimisha Siku hizo mbili kwa pamoja kama ni Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu. Hivyo, Maadhimisho hayo hufanyika mara baada ya Maadhimisho ya (sherehe) za uhuru wa Tanganyika.

Suala la maadili linatuhusu sisi viongozi wote pamoja na watumishi wa umma. Suala hili linahusiana na mienendo na utekelezaji wa majukumu yetu kwa umma tukiwa viongozi na watumishi wa umma. Kadhalika, linahusiana na uwajibikaji, uwazi, mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi, matumizi sahihi ya fedha na rasilimali za umma na usimamizi wa haki za binaadamu.

Kutokana na umuhimu huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha taasisi za kusimamia masuala ya Utawala Bora kwa lengo la kuimarisha utawala bora na maadili kwa viongozi na watumishi wa umma. Taasisi hizo, pamoja na mambo mengine, zimepewa majukumu ya kusimamia maadili ya viongozi wa umma, mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi, usimamizi wa matumizi sahihi ya taratibu za fedha na rasilimali za umma katika taasisi za Serikali pamoja na kuhifadhi, kulinda na kukuza Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora nchini.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Maadhimisho haya pia yamekuwa yakitumiwa na Serikali na Taasisi za Utawala Bora kama njia moja wapo ya kuongeza

uelewa, kwa viongozi, watumishi wa umma pamoja na wananchi kwa ujumla, juu ya umuhimu wa kuimarisha maadili, haki za binadamu, mapambano dhidi ya rushwa, uwazi na uwajibkaji.

Katika kutimiza lengo hilo, Taasisi zinazosimamia Utawala Bora, kuelekea kilele cha Maadhimisho hayo, ziliandaa shughuli mbalimbali ikiwemo utoaji wa elimu, mafunzo na semina kwa wananchi na viongozi wa umma kuhusu umuhimu wa maadili, mapambano dhidi ya rushwa, misingi ya utawala bora na haki za binadamu

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Kauli Mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu wa 2022 ni ***"Tuungane katika kuzuia rushwa, ubadhirifu, wizi wa mali za umma na kukuza maadili, haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa maendeleo ya jamii".***

Kauli mbiu hii inaelezea umuhimu wa kukuza na kuzingatia maadili na misingi ya utawala bora katika utekelezaji wa majukumu ya umma. Hayo yakifanyika, maendeleo ya kweli na ustawi wa wananchi na taifa yataweza kupatikana katika muda mfupi ujao.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Taasisi zinazosimamia Utawala Bora zimeendelea kupata mafanikio na changamoto katika kufanikisha juhudi za Serikali za kuimarisha Maadili na Utawala bora. Njia mbalimbali hutumiwa kukabiliana na changamoto kwa lengo la kuhakikisha kwamba majukumu ya Taasisi yanatekelezwa ipasavyo na kwa ufanisi.

Ninaomba kwa uchache kuelezea baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi (hiki). Taasisi zetu zote zina wajibu wa kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yetu. Hivyo, Elimu kwa Umma imeendelea kutolewa kwa kutumia njia tafauti ikiwemo mikutano ya watendaji, viongozi wa umma na wananchi, majarida na vipindi katika televisheni na radio za vyombo vya habari vya Serikali na Binafsi.

Matokeo ya hatua hii yamesaidia wananchi kujitokeza kuwasilisha malalamiko yao na tuhuma dhidi ya baadhi ya viongozi wa umma kwenye maeneo ya kimaadili, rushwa na uhujumu wa uchumi, mgongano wa kimaslahi, matumizi mabaya ya mali za umma, matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha na kujilimbikizia mali kinyume na sheria. Taasisi zinazohusika na **(malalamiko na tuhuma hizo)** zimeendelea kuyashughulikia kisheria, ambapo malalamiko na tuhuma nyengine utekelezaji wake umekamilika na nyengine zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Kadhalika, kumekuwa na ushirikiano wa kikazi baina ya Taasisi za Utawala Bora za Zanzibar na Taasisi nyengine za Tanzania Bara. Mashirikiano hayo pia yamehusisha baadhi ya Taasisi za kimataifa katika utekelezaji wa majukukumu ya taasisi zetu. Ushirikiano huo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuungwa mkono jitihada za mapambano dhidi ya rushwa nchini, uimarishaji wa maadili, haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Baadhi ya Sheria zilizoanzisha Taasisi zinazosimamia Utawala Bora zimeweka wajibu kwa Taasisi hizo, Kuandaa Ripoti za Mwaka za Utekelezaji wa Majukumu yao. Taarifa ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa kipindi cha Januari hadi Disemba, 2021, Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka 2021/2022 na Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2020/2021, zimeshatayarishwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika.

Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili imeshawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi (AR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman, **jana tarehe 15 Disemba, 2022**.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Mapambano dhidi ya rushwa, ukiukwaji wa maadili, udhalilishaji, uvunjwaji wa haki za binadamu na ubadhirifu wa rasilimali za umma yanahitaji juhudi za pamoja. Hili si suala la kuachiwa Taasisi zinazosimamia utawala bora pekee. Hivyo, Mheshimiwa Mgeni Rasmi, kupitia kwako, kama tulivyokuomba katika Maadhimisho ya mwaka jana, tunazidi kuomba kupatiwa ushirikiano zaidi kutoka kwa viongozi, watumishi wa umma na binafsi pamoja na wananchi ili taasisi zetu ziweze kufikia matarajio na malengo ya kuanzishwa kwake.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Ninaomba, kwa mara nyingine, nitumie fursa hii kukushukuru kwa kukubali kuungana nasi katika Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu, licha ya majukumu mengi yanayokukabili katika kipindi hiki.

Aidha, ninapenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa kamati za maandalizi ya shughuli hii zinazojumuisha watendaji na maafisa kutoka Taasisi zinazosimaia Utawala bora kwa kazi kubwa ya kuandaa sherehe hii, chini ya miongozo ya Watendaji Wakuu wa (AR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Kwa msingi, tunatoa shukrani za dhati kwa Waziri wa Nchi (AR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mwalimu Haroun Ali Suleiman pamoja na Viongozi na watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katiba Mkuu, Nd. Mansura Mosi Kassim. Juhudi za watu wote hao, pamoja na nyinyi waalikwa, ndio zilizofanikisha maadhimisho haya.

Ninapenda pia kuvishukuru vyombo vya habari kwa kuwa daraja baina yetu katika kuwafikishia wananchi taarifa mbali mbali za utendaji wa taasisi zetu na maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu. Vyombo hivi vimekuwa nasi tokea tulipoanza utekelezaji wa shughuli zetu kuelekea kilele cha Maadhimisho haya.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Mwisho ninaomba kuwakumbusha viongozi wenzangu kuwa katika juhudi za Serikali kuimarisha Utawala Bora imeweka utaratibu wa kujaza na kuwasilisha Tume, Fomu ya Tamko la Rasilimali na Madeni si zaidi ya tarehe 31 Disemba, ya kila mwaka. Hadi tarehe ya leo jumla ya viongozi waliorejesha fomu ni **795** sawa na **asilimia 32** Kati ya viongozi **2**,**527** wanaopaswa kuwasilisha fomu hizo. Nikuombe Mhe. Mgeni Rasmi uwakumbushe tena viongozi wa Umma wajibu wao huo ili wasije wakapindukia muda uliowekwa kisheria.

**Mheshimiwa Mgeni** rasmi ninakushukuru tena kwa mara nyengine, na waalikwa wote; Ahsanteni sana; kwa kunisikiliza.

**"*Tuungane katika kuzuia rushwa, ubadhirifu, wizi wa mali ya umma na kukuza maadili, haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa maendeleo ya jamii*".**